

DHIMA NA CHANGAMOTO ZA MATUMIZI YA TAFSIRI KATIKA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI NCHINI UGANDA

Sarah Ndanu M. Ngesu na Leonard Muaka

Ikisiri

Ufundishaji wa lugha ya kigeni au lugha ya pili kwa wanafunzi wenye umilisi wa lugha na desturi zao si jambo rahisi. Wakati mwingine, walimu hutumia tafsiri ili wanafunzi waweze kuelewa vipengele vya lugha ya kigeni inayofundishwa. Makala haya yanaangazia matumizi ya mbinu ya tafsiri katika shule za sekondari jijini Kampala nchini Uganda. Lengo la makala haya ni kujadili iwapo tafsiri inaweza kutambulwa kama stadi ya tano katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Utafiti huu umechochewa na mkanganyiko uliopo kubusu nafasi ya tafsiri katika ufundishaji wa lugha. Ingawa tafsiri hutumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, mbinu hii haibainishwi kama mbinu mojawapo ya ufundishaji kwenye mitaala. Data za utafiti ni za uvandani na maktabani. Data za uvandani zilikusanywa kwa njia ya ushuhudiaji, hojaji na uchambuzi wa nyaraka. Matokeo yanaonesha kwamba tafsiri ni mbinu inayotumiwa kwa upana katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Halikadhalika, makala haya yamebainisha kuwa Kiswahili ni lugha ya kigeni nchini Uganda, hali inayowafanya walimu kutegemea tafsiri baina ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa kubitimisha, makala haya yanashadidia kwamba hata kama tafsiri ina changamoto zake katika ufundishaji wa lugha za kigeni, haiwezi kukwepeka katika ufundishaji wa Kiswahili katika mazingira ambamo lugha hii huitumiwa katika mawasiliano ya kila siku.

Utangulizi

Ufundishaji wa lugha ya kigeni (kuanzia sasa, LGn) kwa wanafunzi wenye umilisi wa lugha na desturi zao si jambo rahisi. Wakati mwingine, walimu hutumia tafsiri ili wanafunzi waweze kuelewa vipengele vya LGn. Mbinu ya tafsiri katika ufundishaji imetumika kwa karne nyingi. Kwa mujibu wa Martin (2013), mwanzoni ufundishaji wa lugha darasani ulianza na tafsiri. Kwa mfano, tafsiri ilitumika katika ufundishaji wa lugha rasimi⁶ kama vile Kilatini na Kigiriki ambapo wanafunzi walihitajika kutumia mbinu ya tafsiri sisizi ili kuimarisha uwezo wao wa kusoma na kuandika pamoja na kutafsiri kazi za

⁶ Tafsiri ya neno 'classical languages'